MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.06. Msimu wa Kilimo 2023/24* *Tathmini ya Novemba 21-30, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 1-10, 2023*

**MUHTASARI**

- Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza, maji kutuama mashambani, na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza wakishirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao.
- Mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za Msimu zitasaidia uoteshaji mbegu na ukuaji wa mazao. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kupanda mbegu mara udongo una-


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2023

Kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika kidogo. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika maeneo ya nchi.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa baharí ya Hindi. Hali hii ilichangia kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2023

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua (milimita kati ya 26 hadi 100 za mvua). Hata hivyo, maeneo machache kuzunguka Ziwa Viktoria na Ziwa Tanganyika yalipata mvua zaidi ya milimita 200 katika dikadi kama inavyoonekana katika Kielelezo 1.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku 10 kwa kipindi cha Novemba 21-30, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2023

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo mengi nchini zilisaidia ukuaji wa mazao. Maeneo yanayopata mvua za vuli hususan pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria mahindi yapo katika hatua mbalimbali za uakuaji, ambapo katika mkoa wa Kagera mahindi yapo katika hatua ya kubumba na kutoa mbelewele.

Kwa upande mwingine, kwa maeneo ya pwani ya kaskazini hususan baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani mahindi yameathirika kidogo kutokana na unyevu mwingi katika udongo.

Ukaushaji wa zao la karafuu umeathiriwa na uwepo wa mvua katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba, hata hivyo vipindi vichache vya ukavu vinavyojitokeza vitasaidia ukaushaji huo.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Msimu waliendelea na upandaji wa mahindi, viazi mviringo na maharage.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama umeanza kuimarika kwa maeneo mengi yanayopata mvua za vuli isipokuwa kwa maeneo machache yanayopata mvua za Msimu hususan kanda ya kati na mkoa wa Iringa ambako hali siyo ya kuridhisha kwa jamii hususan ya wafugaji kutokana na hali ya ukavu iliyopo.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vimeanza kuongezeka hususan kwa mabonde yaliyopo katika maeneo yanayopata mvua za Vuli.

Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka maji yamendelea kupungua katika mabonde mengi kutokana hali ya ukavu iliyopo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo nchini.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2023

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa na mvua katika maeneno machache.

Maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache hususan katika nusu ya kwanza ya dekadi.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2023

Mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za Msimu zitasaidia uoteshaji mbegu na ukuaji wa mazao. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kupanda mbegu mara udongo unapokuwa na unyenyevu wa kutosha.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Vuli wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza, kutuama kwa maji, na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza wakishirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao. Aidha, palizi na matumizi ya pembejeo vinatarajiwa kuathirika kutokana na ongezeko la magugu, vipindi vya mvua na unyevu wa kupitiliza.

Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki, na kuchukua tahadhari kwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi ili kuepuka athari zitokanazo na upepo mkali na mvua kubwa pale vinapojitokeza.

Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya kutosha na kuchimba mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya mifugo yao hususan kwa matumizi ya baadae.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 1-10, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka hususan kwa maeneo yanayopata mvua za vuli kutokana na hali ya mvua inayoendelea. Jamii inashauriwa kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya mafuriko na kuendelea kuimarisha mabwawa. Aidha, maji yaliyopo yatumike kwa uangalifu kufuatia hali ya ukavu iliyopo hususan katika maeneo yanayopata mvua za Msimu ambako mvua bado hazijaanza kunyesha.